BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) 2019

# 721 LUGHA YA KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) MEI, 2019

## 721 KISWAHILI

*Kimechapishwa na;*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

**Haki zote zimehifadhiwa**.

# YALIYOMO


DIBAJI ..... iv

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ..... 2

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalam) ..... 2

2.1.1 Swali la 1: Sarufi ..... 2

2.1.2 Swali la 2: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ..... 5

2.1.3 Swali la 3: Fasihi ..... 8

2.1.4 Swali la 4: Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili ..... 11

2.1.5 Swali la 5: Matamshi na Lafudhi ..... 14

2.1.6 Swali la 6: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ..... 17

2.1.7 Swali la 7: Ufahamu ..... 19

2.1.8 Swali la 8: Upimaji ..... 22

2.1.9 Swali la 9: Maendeleo ya Kiswahili ..... 25

2.1.10 Swali la 10: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili ..... 28

2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma) ..... 31

2.2.1 Swali la 11: Uhakiki wa Kazi za Fasihi ..... 31

2.2.2 Swali la 12: Fasihi ..... 38

2.2.3 Swali la 13: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili ..... 43

2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalam) ..... 47

2.3.1 Swali la 14: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ..... 47

2.3.2 Swali la 15: Upimaji ..... 52

2.3.3 Swali la 16: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ..... 57

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA ..... 63

4.0 HITIMISHO ..... 64

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ..... 65

KIAMBATISHO A ..... 66

KIAMBATISHO B ..... 65

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya mtihani wa Taifa wa kuhitimu mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Sekondari katika somo la Kiswahili mwaka 2019. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani huu.

Taarifa hii inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Majibu ya watahiniwa yanadhihirisha namna watahiniwa walivyofanikiwa au walivyoshindwa kupata maarifa tarajiwa wakati wa mafunzo yao.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kubaini sababu za watahiniwa kufanya vizuri, vibaya au kwa kiwango cha wastani. Baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kufanya vizuri ni kuelewa maelekezo na matakwa ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha na kuwa na uelewa wa mada mbalimbali zilizotahiniwa. Aidha, sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutokufanya vizuri zimefafanuliwa ambazo ni kutokuelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa watahiniwa kujieleza kwa kutumia lugha fasaha, uelewa mdogo wa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili na mada zilizotahiniwa.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua stahiki katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa endapo taarifa hii itafanyiwa kazi ipasavyo, itaboresha kiwango cha kufaulu katika mitihani ya Stashahada ya Ualimu wa Sekondari.

Mwisho, Baraza linapenda kutoa shukrani za dhati kwa maafisa mitihani na wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Charles Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa Stashahada ya Ualimu ulifanyika Mei 2019 kwa kuzingatia muhtasari wa Taaluma na Utaalamu. Mtihani huo ulikuwa na maswali 16 yaliyogawanywa katika sehemu A, B, na C.

Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo kila swali lilikuwa na alama 4. Katika sehemu hii mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote na jumla ya alama ilikuwa ni 40. Maswali ya sehemu hii yalitokana na mada zinazohusu *Taaluma* na *Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili*. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yanayohusu mada za *Taaluma*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) na kila swali lilikuwa na alama 15. Hivyo, jumla ya alama katika sehemu hii zilikuwa 30. Aidha, sehemu C ilikuwa na maswali matatu (3) yanayohusu mada za *Utaalamu* ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) na kila swali lilikuwa na alama 15. Hivyo, jumla ya alama za sehemu hii zilikuwa 30. Kwa ujumla, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali kumi na manne (14) kati ya maswali kumi na sita (16).

Mtihani huu ulikuwa na viwango vitatu vya kufaulu ambapo kiwango kizuri kilianzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu alama 0 hadi 39.

Watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani wa 721 Kiswahili kwa mwaka 2019 walikuwa 1,077. Kati yao, watahiniwa 1064 walifanya mtihani na 13 hawakufanya. Miongoni mwa watahiniwa waliofanya mtihani, waliofaulu kwa daraja A hadi D ni 1,062 sawa na asilimia 99.8 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Aidha, watahiniwa 2 sawa na asilimia 0.2 walipata daraja F. Kiwango hiki cha kufaulu ni kizuri kwa sababu zaidi ya 2/3 ya watahiniwa waliofanya mtihani walipata alama za wastani na zaidi . Hata hivyo, uchambuzi zaidi wa viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa kila swali umefanyika ili kubaini kufaulu kwao. Aidha, chati za viwango vya kufaulu zimeambatanishwa ili kufafanua kufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri cha kufaulu, rangi ya njano wastani na rangi nyekundu ni kiwango hafifu cha kufaulu.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Sehemu hii inahusu uchambuzi wa kina kwa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyofanywa vizuri, wastani na vibaya. Aidha, sababu za kufaulu kwa kila kiwango yaani cha juu, wastani na cha chini kwa watahiniwa zimeelezwa bayana kwa kila swali. Vilevile, sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri au vibaya katika kila swali zimeambatanishwa ili kuonesha majibu sahihi kwa kila swali na majibu yasiyo sahihi.

Swali litaelezwa kwamba limejibiwa vizuri ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa wamelijibu vizuri na kupata alama za juu na litaelezwa kuwa limejibiwa vibaya ikiwa theluthi (1/3) tu ya watahiniwa ndio waliolijibu vizuri. Aidha, swali litaelezwa kuwa limejibiwa kwa wastani ikiwa idadi ya watahiniwa waliojibu vizuri inazidi theluthi moja (1/3) na haikuzidi theluthi mbili (2/3).


## 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalam)

Sehemu hii ilikuwa na maswali kumi (10) yaliyohitaji majibu mafupi ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma* na *Utaalam*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na uzito wa alama nne (4) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama arobaini (40). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 1.5, 2 hadi 2.5 wastani na alikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu iwapo alipata alama 3 hadi 4.

### 2.1.1 Swali la 1: Sarufi


Swali hili lilihusu mada ya Sarufi na lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu kauli mbalimbali za utendaji katika lugha ya Kiswahili. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi kauli nne za utendaji katika lugha ya Kiswahili na lilikuwa alama 4.

Asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili kwa kuwa lilikuwa ni la lazima. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa sababu asilimia 66.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 3 inafafanua viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 1:***Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 1.*

Asilimia 43.8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walifanikiwa kueleza kwa ufasaha kauli tatu au zote nne za utendaji katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya kauli sahihi zilizotolewa ni pamoja na *kauli ya kutenda, kauli ya kutendana, kauli ya kutendea na kauli ya kutendewa*. Watahiniwa wengine waliweza kueleza kwa usahihi kauli nyingine za utendaji katika lugha ya Kiswahili ambazo ni kauli ya *kutendwa*, *kutendesha*, *kutendeka na kutendua*. Watahiniwa hao walijibu kwa usahihi kwa sababu katika lugha ya Kiswahili kuna kauli nyingi za utendaji. Mafanikio hayo yalichagizwa na umahiri wa watahiniwa hao juu ya mada ya *Sarufi* na kuelewa matakwa ya swali kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.1.1.



i/ Kauli ya kutenda, huonesha na
mna mtenda jambo anavyotenda kitend
o katika sentensi mfano:- Ninaandika

ii/ kauli ya kutendwa, huonesha namn
a tendo lilivyofanyika au alivyofanyiwa
mtu au kitu fulani
Mfano :- Mussa Amepigwa


ii/ Kauli ya Kutendewa, huonesha kitendo
alichofanyiwa mtu au kitu kwa niaba
yake mfano :- Mama amenipikia chakula

iii/ Kauli ya Kutendana, huonesha namna
ambavyo watu wanavyoweza kufanyia
na jambo fulani kwa pamoja
Mfano Juma na Asha wanapigana

**Kielelezo Na. 1.1:** Majibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Katika kielelezo Na. 1.1 mtahiniwa ameweza kuelezea kwa kifupi kauli nne za utendaji katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi.

Vilevile, watahiniwa 352 sawa na asilimia 33.1 walijibu swali hili na kupata alama hafifu ambazo ni 0 hadi 1.5. Baadhi yao, walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na umahiri wa kutosha juu ya mada ya *Sarufi* hususan mada ndogo ya *Kauli mbalimbali za vitenzi*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kinyume kabisa na matakwa ya swali kwani alieleza stadi nne za lugha ambazo ni *Kusoma, Kusikiliza, Kuandika na Kuzungumza* badala ya kauli nne za utendaji katika lugha ya Kiswahili ambazo ni: *kauli ya kutenda, kutendwa, kutendana, kutendewa, kutendeka, kutendea, kutendesha na kutendua*. Aidha, katika mfano mwingine mtahiniwa mmoja alieleza hali za vitenzi vya Kiswahili ambazo ni *hali ya maelezo, swali, amri na mshangao*. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuelewa matakwa ya swali kwa kueleza stadi nne za lugha badala ya kauli nne za utendaji katika lugha ya Kiswahili.


(i) Kusoma: Ni moja ya kauli katika lugha ya Kiswahili ambayo huweza kusaidia katika kubuni idadi ya wanaojua kusoma katika fimo la Kiswahili.

(ii) Kusikiliza: Ni moja ya kauli katika lugha lugha ya Kiswahili ambapo mtu hukaa mtoka kuwa msikivu katika jambo fulani.

(iii) Kuandika: Ni moja ya kauli ambapo mtu hupimwa kabla ya kuingia darasa fulani kama anajua au hajui kuandika.

(iv) Kuongea: Ni moja ya kauli katika lugha ya Kiswahili ambapo mwanafunzi hulazimika kuongea kwa kutumia lugha fasaha.

**Kielelezo Na. 1.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


Katika kielelezo Na. 1.2 mtahiniwa ameleza stadi nne za lugha badala ya kauli nne za utendaji katika lugha ya Kiswahili.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 23.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliweza kutaja kwa usahihi kauli nne za utendaji katika lugha ya Kiswahili bila kuelezea kwa kifupi na wengine walielezea kwa kifupi kauli mbili badala ya nne na kusababisha kupata alama za wastani.

### 2.1.2 Swali la 2: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia*. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa juu ya mbinu ya vikundi vya majadiliano ambapo mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa kifupi kanuni nne zitakazofuatwa wakati mwalimu anaendesha vikundi vya majadiliano darasani.


Swali lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 72.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifanya vizuri na kupata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na.** *2:Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali 2.*

Watahiniwa 594 sawa na asilimia 55.8 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hao waliweza kueleza kanuni tatu au nne zitakazofuatwa wakati mwalimu anaendesha vikundi vya majadiliano darasani kwa kutoa hoja kama: *Kuwa na viongozi wa vikundi (wenyeviti na makatibu), mwalimu awapange wanafunzi katika makundi yao kulingana na uwezo wao, kupanga kazi itakayofanyika katika kila kundi na mwalimu anatakiwa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki kufanya kazi katika kundi husika*.


Aidha, watahiniwa wengine waliandika hoja nyingine kama: *mwalimu azungukie vikundi ili kuelekeza au kusaidia wanafunzi wanapohitaji msaada, mwalimu atoe muda wa kutosha wa majadiliano kulingana na swali au maswali aliyowapa wanafunzi, mwalimu asitishe majadiliano na kutoa muda kwa makatibu wa makundi kuwasilisha majibu huku yeye akiandika majibu hayo ubaoni na mwisho mwalimu atoe hitimisho na majibu sahihi*. Watahiniwa hao waliweza kueleza kanuni hizo kwa usahihi kwa kuwa walikuwa na umahiri wa kutosha katika mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia* kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 2.1.


2. i) Kuwagawa wanafunzi katika makundi
madogo madogo. Hapa mwalimu anafanya kazi
ya kuwapanga wanafunzi katika vikundi.
ii) Kutoa mada itakayojadiliwa kwa
kila kikundi. Mwalimu anatakiwa kuta
mbulisha mada ambayo inatakiwa kujadili
wa na wanafunzi.
iii) Kuhakikisha kuwa kila kikundi
kuna kiongozi. Ni lazima pawepo na
na kiongozi wa kikundi jambo mwali
mu yeye ni msimamizi mkuu.
iv) Kuhakikisha kila mwanafunzi anash
riki vyema. Hapa mwalimu anapaswa
kuhakikisha kuwa anasimamia vyema maku
ndi na kuona jinsi ambavyo kila mwanafunzi
anashiriki.

**Kielelezo Na. 2.1**: Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 2.1 mtahiniwa ameeleze kanuni sahihi za kufuatwa wakati mwalimu anaendesha vikundi vya majadiliano darasani kwa usahihi.

Vilevile, asilimia 28.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5. Miongoni mwa sababu zilizochangia ufaulu hafifu ni pamoja na kukosa uelewa juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia*. Baadhi ya watahiniwa walikosa maarifa katika mada husika.Hii ilipelekea kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kupata alama hafifu. Vilevile, watahiniwa wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali ambapo walichanganya maarifa na kutoa hoja zilizotofautiana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mambo ya msingi anayotakiwa kuzingatia mwanafunzi awapo darasani kama vile *utulivu, usikivu na umakini* hivyo kupata alama 0. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.


2. i/ Utulivu
ii/ Usikivu
iii/ Mjadala
iv/ Umakini.

**Kielelezo Na. 2.2**: Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


Majibu ya mtahiniwa katika Kielelezo Na. 2.2 yanaonesha kuwa alishindwa kueleza kanuni zitakazofuatwa wakati mwalimu anaendesha vikundi vya majadiliano darasani badala yake akataja mambo ya msingi anayotakiwa kuzingatia mwanafunzi awapo darasani.

Hata hivyo, asilimia 16.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliweza kutaja kanuni nne za kuendesha vikundi vya majadiliano darasani bila kutoa ufafanuzi kwa ufupi kama swali lilivyoelekeza. Aidha, watahiniwa wengine waliweza kufafanua kanuni mbili tu kwa usahihi badala ya nne na wengine walitaja kanuni zote kwa usahihi na kuchanganya maelezo ya kanuni walizozitaja hivyo kupata alama pungufu.

### 2.1.3 Swali la 3: Fasihi

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Fasihi*. Swali lilikuwa na vipengele viwili ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi maana ya vipera vya maigizo kwa kutumia mfano ambavyo ni (a) Majigambo na (b) Tambiko. Swali lilikuwa na jumla ya alama 4 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2.


Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Asilimia 58.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani. Uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kumefafanuliwa vizuri katika chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 3.*

Watahiniwa 442 sawa na asilimia 41.5 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao hawakuwa na uelewa sahihi juu ya mada ya *Fasihi* hususan mada ndogo ya *Fasihi simulizi katika kipengele cha tanzu za fasihi simulizi* na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana ya majigambo kuwa ni *hadithi zinazomuelezea kiumbe au mtu kutoka katika jamii fulani*. Mtahiniwa huyu alishindwa kuelewa kuwa majigambo sio hadithi bali ni tendo la *msanii au fanani kujisifu na kujifaragua ambapo kujisifu huko kunaweza kuwa juu ya mafanikio yake katika kugombea wadhifa fulani au juu ya historia yake. Kwa mfano, anaweza akajigamba kwa sababu ana utajiri mwingi kama vile ng'ombe wengi au mashamba mengi*.

Aidha, alieleza maana ya tambiko kuwa *ni hadithi zinazohusiana na mila na desturi za jamii fulani* badala ya *sadaka inayoambatana na imani za kitamaduni inayotolewa kwa miungu kupitia kwa wahenga, mizimu, mahoka au pepo. Kwa mfano kuchinja wanyama wakati wa kuomba mvua*. Pamoja na hayo, mtahiniwa huyo alitumia msamiati kutambika unaotakiwa kutolewa maana katika maelezo yake na hivyo kupata alama 0. Vilevile, watahiniwa wengine walishindwa kutoa mifano sahihi katika maana walizotoa dosari iliyopelekea kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kutokana na uelewa mdogo juu ya mada iliyotahiniwa na kupata alama hafifu.



3. a) Majigambo
Ni hadithi zinazomuelezea kuimbe au mtu kutoka
na na alivyo yeye mwenyewe. Mara nyingi majigambo
huelezea jinsi watu walivyo Kwamfano Mwalimu J. K
Nyelele alikuwa ni mtu wa kwanza kuleta uhuru katika
Tanganyika.

b) Tambiko
Ni hadithi zinazohusiana na mila na desturi
za jamii fulani. Mara nyingi watu wa jamii fulani
wanaweza kutambika ili waweze kujikinga na kitu
fulani katika kijiji chao kinachowazunguka.

**Kielelezo Na. 3.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa alipata alama hafifu kutokana na kushindwa kutoa maana sahihi ya vipera vya maigizo na kuweka mifano.

Hata hivyo, asilimia 31.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri kwa sababu waliweza kutoa maana sahihi ya vipera vya maigizo ambavyo ni majigambo na tambiko huku maana hizo zikishadidiwa vyema na mifano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana ya majigambo kuwa ni *moja ya kipera cha maigizo ambacho kinaelezea hali ya kujikweza kwa mabavu mbele ya hadhira na kujipa sifa nyingi* na akatoa mfano "*mimi ni simba hapa mtaani kote naogopeka kwani naweza kumrarua binadamu yeyote*". Aidha, alielezea tambiko kuwa ni *sherehe za kijadi zifanywazo na wanajamii mwisho wa mwaka kwa ajili ya kutoa sadaka kwa miungu yao*. Majibu sahihi yaliyotolewa katika swali hili yanadhihirisha kuwa, watahiniwa wa kundi hili walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada ya *Fasihi*. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutoa maana sahihi ya vipera vya maigizo kwa mifano.





**Kielelezo Na. 3.2 :** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kutoa maana sahihi ya vipera vya maigizo ambavyo ni majigambo na tambiko huku maana hizo zikishadididiwa vyema na mifano na kupata alama za juu.

### 2.1.4 Swali la 4: Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze kwa kifupi sifa kuu nne za muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari.


Watahiniwa wote 1,064 waliofanya mtihani walijibu swali hili kwa kuwa lilikuwa ni la lazima. Swali hili lilijibiwa kwa kiwango cha wastani kwa sababu asilimia 57.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani walipata alama za wastani na zaidi. Kufaulu kwa watahiniwa hao kiasilimia kumewasilishwa vizuri katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 4.*

Watahiniwa 487 ambao ni sawa na asilimia 45.8 walimudu kwa wastani kueleza sifa kuu nne za muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari. Vilevile, watahiniwa hawa hawakutoa maelezo ya kuridhisha katika kujibu swali husika na wengine walieleza sifa mbili sahihi na nyingine hazikuwa sahihi. Hivyo, walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5.


Hata hivyo, asilimia 42.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Hii ilitokana na baadhi ya watahiniwa kukosa uelewa wa kutosha juu ya mada ya Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili hivyo kuchanganya hoja sahihi na zisizosahihi na kusababisha kupata alama hafifu. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali dosari iliyosababisha kuchanganya umuhimu, sifa na dhima za muhtasari wa somo la Kiswahili na kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza namna muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari unavyomsaidia mwalimu katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa hoja kama: *kurahisisha ufundishaji, kuandaa azimio na andalio la somo na kumsaidia mwalimu kuchagua mbinu na zana za kufundishia* badala ya kueleza kwa kifupi sifa kuu nne za muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari ambazo ni: *Uoneshe malengo ya jumla ya elimu ya sekondari, Uoneshe malengo ya jumla ya somo la Kiswahili, Uoneshe malengo ya elimu Tanzania na Ubainishe ujuzi wa jumla wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari*. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha kati ya sifa za muhtasari wa somo la Kiswahili na umuhimu wa muhtasari huo.


4. Muhtasari, Ni muongozo wa mambo au mada zilizopangiliwa kufundishwa katika darasa fulani kwa muda wa mwaka mzima. Zifuatazo ni sifa za muhtasari wa somo la kiswahili kwa shule za Sekondari:
Kumsaidia mwalimu katika kuandaa azimio la kazi na andalio la somo, Muhtasari ni muhimu sana katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji.
Kumsaidia mwalimu kuchagua njia bora na mbinu bora za kufundishia na kujifunzia, Muhtasari humsaidia mwalimu katika kujua njia bora za kufundishia mada fulani.
Humsaidia mwalimu kuchagua zana bora za kufundishia na kujifunzia, Muhtasari ni muhimu sana katika kuchagua zana zitakazotumika kufundishia na kujifunzia kulingana na mada husika.
Humsaidia mwalimu kujua mada kuu na mada ndogo za kufundishia, Muhtasari humuongoza mwalimu ili aweze kufundisha mada zote kwa ustadi.

**Kielelezo Na. 4.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha kuwa mtahihiniwa alijibu kinyume na matakwa ya swali kwa sababu alielezea namna muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari unavyomsaidia mwalimu katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji badala ya kueleza kwa kifupi sifa kuu nne za muhtasari huo.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 11.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walifanya vizuri kwa kupata alama 3 hadi 4. Ufaulu huo ulitokana na uwezo mzuri wa kueleza sifa kuu tatu au nne za muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari. Hoja zilizoelezwa ni pamoja na: *Uoneshe malengo ya jumla ya elimu ya sekondari, Uoneshe malengo ya jumla ya somo la Kiswahili, Uoneshe mbinu mbalimbali zitakazotumika kufundisha mada mbalimbali* na *huonesha vipindi vitakavyotumika kufundisha mada za somo la Kiswahili*. Hii inaonesha kuwa, watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



04 i) Huonesha malengo ya jumla ya elimu ya sekondari.
ii) Huonesha malengo ya jumla ya somo la Kiswahili kwa shule za sekondari.
iii) Huonesha mbinu zitakazotumika kufundisha somo la Kiswahili.
iv) Huonesha vipindi vitakavyotumika kufundisha mada za somo la Kiswahili.


**Kielelezo Na. 4.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Majibu katika kielelezo Na. 4.2 yanaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kueleza kwa kifupi sifa nne za muhtasari wa somo la Kiswahili kwa usahihi.

### 2.1.5 Swali la 5: Matamshi na lafudhi


Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Matamshi na lafudhi*. Swali lilikuwa na vipengele viwili ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi maana ya vitamkwa vya Kiswahili kwa kutumia mifano ambavyo ni (a) Irabu na (b) Konsonanti. Swali lilikuwa na jumla ya alama 4 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2.

Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 85.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4. Kufaulu kwa watahiniwa kumefafanuliwa vizuri katika chati Na. 5 kiasilimia.




***Chati Na. 5:*** *Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 5.*

Watahiniwa wengi sawa na asilimia 56.9 waliojibu swali hili walijibu vizuri na kupata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao waliweza kueleza maana ya vitamkwa vya Kiswahili na kutoa mifano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana ya irabu kuwa *ni aina ya vitamkwa ambavyo hutolewa pasi na kuwepo kizuizi chochote kwenye mkondohewa utokao mapafuni kupitia kwenye chemba ya kinywa na chemba ya pua mfano: a, e, i, o, u*. Halikadhalika, alieleza maana ya *Konsonanti* kuwa ni *vitamkwa ambavyo hutolewa kwa kuwepo vizuizi kwenye mkondo wa hewa kutoka mapafuni, ukipitia chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje. Mfano: n, m, t, k*. Hii inadhihirisha kwamba watahiniwa wa kundi hili walielewa vizuri mada iliyotahiniwa. Tofauti ya alama kati ya watahiniwa wa kundi hili ilitokana na ufasaha katika kujieleza na mifano sahihi. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


5 (a) Irabu
Ni sauti zinazotamkwa bila Kuwepo
Kizuizi chochote cha mkondo wa hewa
Kutoka mapafuni Kwenda nje Kupitia chembe
Kinywa na pua.
mfano wa irabu ni a, e, i, o, u

(b) Konsonanti
Ni sauti zinazotamkwa Kwa Kuwepo
Kizuizi cha mkondo wa hewa
Kutoka mapafuni Kwenda nje
Kupitia chembe ya Kinywa na pua
Mfano p, B, z


**Kielelezo Na. 5.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kueleza kwa kifupi maana ya vitamkwa vya Kiswahili na kutoa mifano kutokana na uelewa wa kutosha aliokuwa nao juu ya mada ya *Matamshi na Lafudhi*.

Baadhi ya watahiniwa walishindwa kutoa maana zilizojitosheleza na mifano sahihi. Wengine waliweza kutoa maana sahihi lakini mifano ikakinzana na maana walizotoa na kati yao walitoa maana zisizojitosheleza lakini mifano ikawa sahihi hivyo kupata alama za wastani. Kundi hili ni asilimia 28.8 ya watahiniwa wote waliofanya swali hili ambao walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5.

Aidha, asilimia 14.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Matamshi na Lafudhi*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika maana ya irabu kuwa *ni muunganiko wa silabi*. Maana ya irabu iliyotolewa ni maelezo yanayoelezea maana ya neno kwa kuwa neno ndilo linaloundwa na muunganiko wa silabi. Hivyo basi, kutoa maana ya neno katika kueleza maana ya irabu kunaonesha bayana kuwa, mtahiniwa huyo hakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada iliyotahiniwa. Vilevile, alieleza maana ya konsonanti kuwa *ni muunganiko wa Irabu* ilihali konsonanti *ni vitamkwa ambavyo*

*hutolewa kwa kuwepo kizuizi kwenye mkondo wa hewa kutoka mapafuni, ukipitia chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje*. Mtahiniwa huyu alichanganya maana ya neno na konsonati kwa sababu neno ndilo huweza kuundwa kwa muunganiko wa irabu na si konsonanti. Halikadhalika, alishindwa kutoa mifano kama swali lilivyoelekeza na baadhi ya maneno hayakuandikwa kwa usahihi katika maana zilizotolewa kwa mfano, neno “silabi” liliandikwa “sirabi” na “konsonanti” liliandikwa “consonanti”. Watahiniwa wengine katika kundi hili walichanganya maarifa na hivyo kuchanganya maana sahihi na zisizo sahihi na kusababbisha kupata alama za chini. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


5. (a) Irabu ni Muunganiko wa sirabi

(b) consonanti ni Muunganiko wa irabu.


**Kielelezo Na. 5.2:** Majibu ya  mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa alishindwa kutoa maana sahihi za vitamkwa vya Kiswahili kwa kutumia mfano .

### 2.1.6 Swali la 6: Zana za Kufundishia na Kujifunzia


Swali hili lilihusu mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*. Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kuainisha njia nne zinazoweza kumsaidia mwalimu kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa urahisi.

Watahiniwa wote 1,064 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Asilimia 84.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu kwa asilimia.




*Chati Na. 6:* *Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 6.*

Watahiniwa 899 sawa na asilimia 71.9 walijibu vizuri swali hili kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*. Vilevile, watahiniwa hao walielewa vizuri matakwa ya swali hivyo waliweza kuainisha kwa usahihi njia tatu au nne zitakazomsaidia mwalimu kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa urahisi. Miongoni mwa hoja sahihi zilizotolewa ni kama: *Kununua*, *Kutengeneza*, *Kuazima, na Kukusanya*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.



06 i) Kutengeneza. Mfano. Vyungu, Michoro
ii) Kutokana katika mazingira ya kawaida. Mfano Matunda.
iii) Kununua. Mwalimu hununua kutoka maeneo mbalimbali. Mfano dukani.
iv) Kuazima Kutoka kwa wengine

**Kielelezo Na. 6.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kuainisha njia nne zinazoweza kumsaidia mwalimu kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa urahisi.

Hata hivyo, asilimia 15.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao, hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kwa kubuni tu ambayo hayahusiani na swali, majibu yaliyotolewa ni pamoja na *ubunifu, ujuzi, vifaa na kutenda* badala ya njia nne zinazoweza kumsaidia mwalimu kupata zana kwa urahisi kama vile *Kununua, Kutengeneza, Kuazima, na Kukusanya.*

Vilevile, wapo watahiniwa wachache waliandika faida za kutumia zana wakati mwalimu anapokuwa anafundisha darasani na kupata alama 0. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama: *kurahisisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji, husaidia wanafunzi kutunza kumbukumbu ya kudumu, huwashirikisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na huandaa wanafunzi kuwa wabunifu kutokana na kushirikishwa kutengeneza zana hizo.* Aidha, wapo watahiniwa ambao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada husika hivyo kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na kusababisha kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.


6 i) Ubunifu
ii) Ujuzi
iii) Vifaa
iv) Kutenda.

**Kielelezo Na. 6.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


Majibu katika kielelezo Na. 6.2 yanaonesha kuwa mtahiniwa alishindwa kuainisha njia nne za kumsaidia mwalimu kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa urahisi.

Vilevile, asilimia 12.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu waliweza kupata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5 kutokana na kutoa hoja chache, kurudia hoja yenye maana moja na kuchanganya hoja sahihi na zisizosahihi.

### 2.1.7 Swali la 7: Ufahamu


Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Ufahamu*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne zinazobainisha umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu katika shule za sekondari. Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya

watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 92.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 7 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




***Chati Na. 7:*** *Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 7.*

Watahiniwa 720 sawa na asilimia 67.7 walipata alama za juu ambazo ni kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hao waliweza kukidhi matakwa ya swali kutokana na uelewa mkubwa waliokuwa nao juu ya mada ya *Ufahamu*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha hoja tatu sahihi zinazoonesha umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu katika shule za sekondari kuwa ni: *humsaidia mwanafunzi kujua matumizi ya alama za uandishi, kukuza stadi za kusoma kwa sauti na kusoma kimya na kukuza stadi za kusikiliza, kutafakari na kuandika*. Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika hoja nyingine kama vile *kumwezesha mwanafunzi kujitahini, kuelewa na kutathmini mawazo ya mwandishi na kukuza au kuendeleza tabia ya usomaji*. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu katika shule za sekondari na kupata alama za juu.



7. i. Humsaidia mwanafunzi kujua matumizi ya alama za uandishi kama vile, mkato nukta, alama za mshangao na alama za kuuliza.

ii. Humsaidia mwanafunzi kukuza stadi ya kusoma kwa sauti na kusoma kimya kwa kutumia habari mbalimbali.

iii. Husaidia Mwanafunzi kufupisha habari ndefu kwa kutumia maneno machache.

iv. Humsaidia mwanafunzi kukuza stadi ya kutafakari, kusikiliza na kuandika habari mbalimbali kwa usahihi baada ya kusoma makala ya ufahamu.


**Kielelezo 7.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi

Kielelezo 7.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kubainisha hoja tatu zinazoonesha umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu katika shule za sekondari. Aidha, hoja (iii) haikuwa sahihi.

Vilevile, watahiniwa 267 sawa na asilimia 25.1 walipata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5 kwa kuwa walitoa maelezo ambayo si toshelevu. Wengine walitoa hoja mbili sahihi badala ya nne na kushindwa kuonesha kwa kifupi jinsi ambavyo somo la ufahamu ni muhimu kufundishwa katika shule za sekondari.

Aidha, watahiniwa 77 ambao ni asilimia 7.2 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa sababu hawakujibu kulingana na matakwa ya swali. Mfano, mtahiniwa mmoja alieleza faida za mwanafunzi kusoma habari mbalimbali kama vile *Husaidia kumkosoa mwanafunzi, husaidia kumuonya mwanafunzi, husaidia kumuelimisha mwanafunzi na husaidia kumburudisha mwanafunzi* badala ya kubainisha umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu katika shule za sekondari ambao ni *Humsaidia mwanafunzi kujua matumizi ya alama za uandishi*, *Kukuza stadi za kusoma kwa sauti na kusoma kimya*, *Kumwezesha*

*mwanafunzi kujipima na kukuza ,kuendeleza tabia za usomaji na kutathmini na kuelewa mawazo ya mwandishi* na hivyo kupata alama 0. Vilevile, baadhi ya watahiniwa walieleza hatua za kufundisha somo la ufahamu ambazo ni *utangulizi, maarifa mapya, kukazia maarifa,tafakuri na hitimisho*. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama hafifu.


7 (i) Husaidia kumkosoa mwanafunzi.
(ii) Husaidia kumuonya mwanafunzi.
(iii) Husaidia kumwelimisha mwanafunzi.
(iv) Husaidia kumburudisha mwanafunzi.


**Kielelezo 7.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Majibu katika Kielelezo 7.2 yanaonesha kuwa mtahiniwa alishindwa kujibu kulingana na matakwa ya swali kwa kueleza faida za mwanafunzi kusoma habari mbalimbali badala ya umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu katika shule za sekondari.

### 2.1.8 Swali la 8: Upimaji

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Upimaji* hususan mada ndogo ya *Aina na Matumizi ya Upimaji*. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi mambo manne ambayo mwalimu anaweza kuyapima wakati anafundisha darasani.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya. Asilimia 17.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili ndio waliopata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 8 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




***Chati Na. 8:*** *Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 8.*

Watahiniwa 881 sawa na asilimia 82.8 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Upimaji*. Pia, hawakuweza kutimiza matakwa ya swali kwani wengi wao walishindwa kueleza kwa kifupi mambo manne ambayo mwalimu anaweza kuyapima wakati anafundisha darasani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza stadi nne za lugha ambazo ni *stadi ya kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza* badala ya kueleza mambo manne ambayo mwalimu anaweza kuyapima wakati anafundisha darasani ambayo ni *mbinu za kufundishia na kujifunzia, malengo mahsusi ya somo, zana/vifaa vya kujifunzia na vitendo/nyenzo za upimaji alizotumia*. Katika mfano mwingine mtahiniwa mmoja alieleza kwa kifupi aina za upimaji ambazo ni *Upimaji wa awali, Upimaji endelevu na Upimaji tamati*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali na hivyo kupata alama 0.

08 i. Stadi za kuandika; wakati wa kufundisha darasani mwalimu anaweza kupima stadi za kuandika kwa wanafunzi kwamba je wanauwezo wa kuandika au la.

ii. Uwezo wa kusoma; mwalimu anaweza kupima uwezo walionao wanafunzi katika kusoma.

iii. Stadi za kujieleza kwa kina na kwa ufasaha; mwalimu anweza kupima uwezo wa kujieleza kwa kina na kwa ufasaha kwa wanafunzi wakati wa kufundisha.


iv. Stadi za kusikiliza; mwalimu anaweza kupima stadi za kusikiliza kwa wanafunzi wakati wa kufundisha darasani.

**Kielelezo Na. 8.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliandika stadi za lugha badala ya kueleza kwa kifupi mambo manne ambayo mwalimu anaweza kuyapima wakati anafundisha darasani .

Vilevile, asilimia 11.4 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walishindwa kutoa hoja zinazojitosheleza kimaelezo na baadhi ya hoja walizotoa hazikuwa sahihi. Vilevile walichanganya hoja, kwa mfano mtahiniwa mmoja alichanganya mambo ambayo mwalimu anaweza kuyapima wakati anafundisha darasani kama vile *uelewa wa wanafunzi* na *mbinu ya kufundishia aliyotumia* na faida za mwalimu kujipima wakati anafundisha darasani ambazo ni: *humsaidia mwalimu kuboresha mbinu aliyotumia na humpa mwalimu ari ya kuendelea na somo linalofuata*.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 5.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa wa kundi hili waliweza kueleza mambo ambayo mwalimu anaweza kuyapima wakati anafundisha darasani. Uwezo huu ulitokana na umahiri walioupata kwenye mada ya *Upimaji*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza mambo hayo kuwa ni: *kutathmini uelewa wa wanafunzi, mbinu iliyotumika kufundishia na Kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia na malengo mahsusi ya somo*. Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kulingana na matakwa ya swali.


8. Mambo ambayo Mwalimu anaweza Kupima darasani.
i/ Uelewa wa wanafunzi
Hapa mwalimu anaweza Kupima Kwa Kuwauliza wanafunzi maswali
ii/ Mbinu ya Kufundishia
mwalimu anaweza Kupima mbinu aliyotumia Kama imefanikiwa au haijafanikiwa.
iii/ Zana aliyotumia
Mwalimu anaweza Kupima zana aliyo tumia Kama imeweza Kueleweka Kwa wanafunzi
iv/ Lengo la somo
Mwalimu akiwa darasani anaweza Kupima lengo lake Kama limeweza Kufikia Kwa Kuwauliza wanafunzi maswali.

**Kielelezo Na. 8.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.


Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kueleza mambo manne ambayo mwalimu anaweza kuyapima wakati anafundisha darasani kwa usahihi.

### 2.1.9 Swali la 9: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususan mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki*. Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kufafanua hoja mbili zinazoonesha namna


ambavyo harakati za kisiasa zilivyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili Tanganyika kabla ya uhuru.

Watahiniwa 1,064 waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 85.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 9 inafafanua viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika asilimia.




***Chati Na. 9:*** *Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 9.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 48.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu walizingatia matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kufafanua namna harakati za kisiasa zilivyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili Tanganyika kabla ya uhuru. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa *harakati za kisiasa zilipamba moto baada ya kuzaliwa chama cha TANU ambacho kilitumia lugha ya Kiswahili kwenye shughuli zake na Kiswahili kilihusishwa na umoja, uzalendo na uhuru hivyo kuonekana kama lugha ya ukombozi*. Mtahiniwa huyo aliweza kuonesha bayana mambo yanayohusiana na harakati za kisiasa huku akihusisha na kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Hii inaonesha kwamba, watahiniwa wa kundi hili walielewa vizuri matakwa ya swali. Kielelezo 9.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


9. Harakati za kisiasa
i) Kipindi cha kudai uhuru harakati
za kisiasa zilisaidia sana katika
kukuza na kueneza kiswahili
mfano chama cha TANU kilisaidia
sana kuhamasisha na kutumia
lugha ya kiswahili akiwemo
Mwalimu Nyerere

ii) Kipindi cha kuhamasisha umoja
Tanganyika, ilitumia lugha
ya kiswahili na kiliunganisha
makabila yote. Hivyo kilienea
kwa urahisi


**Kielelezo Na. 9.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na**.** 9.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kufafanua kwa usahihi namna harakati za kiasa zilivyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili Tanganyika kabla ya uhuru.

Vilevile, asilimia 36.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwani walieleza hoja moja sahihi badala ya mbili kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Wengine walizungumzia hoja moja kabla ya uhuru kama: *kuanzishwa kwa gazeti maalum*, *kuzaliwa kwa chama cha TANU au kuanzishwa kwa radio ya sauti ya Dar es saalam* na kuchanganya hoja nyingine isiyohusiana na harakati za kisiasa kama: *mwingiliano kati ya waarabu* na *watu walioishi Pwani ya Afrika Mashariki na biashara.*

Hata hivyo, asilimia 14.9 walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao walichanganya hoja za kabla, wakati na baada ya uhuru na wengine walitoa hoja ambazo hazihusiani kabisa na jinsi harakati za kisiasa zilivyosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili Tanganyika kabla ya uhuru. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuhusu *maswala ya dini* na *maswala ya biashara*. Majibu ya mtahiniwa huyu yanaonesha kushindwa

kabisa kuhusianisha kati ya harakati za kisiasa na kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili kabla ya uhuru. Pamoja na hayo, alishindwa kuelezea hoja zake katika mtiririko unaoleta mantiki na kusababisha hoja hizo kutokueleweka. Hii ilichagizwa zaidi na uelewa mdogo wa mada na kutokuelewa matakwa ya swali. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali na kupata alama 0.


09. (i) Masuala ya dini: wageni baada ya kufika Afrika walitumia siasa ya kueneza dini ya kislamu mfano walifundisha madrasa dini ya kislamu kwa kutumia lugha kiswahili
(ii) Masuala ya biashara: walitumia siasa ya uongozi kufanya biashara na waafrika kwa kutumia lugha ya Kiswahili na kueneza lugha.


**Kielelezo 9.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Maelezo katika kielelezo 9.2 yanaonesha kuwa mtahiniwa alieleza jinsi masuala ya dini na biashara yalivyokuza na kueneza Kiswahili badala ya kueleza jinsi harakati za kisiasa zilivyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

### 2.1.10 Swali la 10: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili


Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* hususan mada ndogo ya *Andalio la Somo*. Swali lilimtaka mtahiniwa abainishe mambo manne anayoweza kuyafanya mwalimu katika hatua ya utangulizi wakati akifundisha mada ya chimbuko la Kiswahili.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani. kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni cha wastani kwa kuwa asilimia 42.5 walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 10 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




***Chati Na. 10:*** *Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 10.*

Watahiniwa 611 sawa na asilimia 57.5 walijibu swali hili na kupata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0.5 hadi 1.5 kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* hivyo kushindwa kubainisha mambo mahsusi ambayo mwalimu anaweza kuyafanya katika hatua ya utangulizi anapofundisha mada ya chimbuko la Kiswahili. Mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha mambo hayo kuwa ni: *kutoa hadithi fupi inayohusu kuja kwa waarabu, kuandika misamiati miwili au mitatu inayotokana na lugha za makabila, kufafanua maana ya lugha na kuelezea ujio wa wakoloni katika Afrika* badala ya *kujenga utayari kwa wanafunzi kupokea maarifa, kuuliza maswali mafupi kuhusiana na mada ya chimbuko la kiswahili, kutoa muhtasari wa somo analotaka kulifundisha(chimbuko la Kiswahili) na kuuliza maswali mafupi yanayohusiana na mada iliyopita* na kupata alama 0.5. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha mambo manne anayoweza kuyafanya mwalimu katika hatua ya utangulizi wakati akifundisha mada ya chimbuko la Kiswahili.




10 i/ Kutoa hadithi fupi inayohusu kuja kwa waarabu katika Pwani ya Afrika Mashariki,
ii/ Kuandika misamiati miwili au mitatu inayotokana na Lugha za makabila tofauti ili kuona upatanisho wa kisarufi katika maneno hayo
iii/ Kufafanua Maana ya Lugha,
iv/ Kuelezea ujio wa wakoloni katika Afrika Ikiwemo Afrika Mashariki, katika nyanja za biashara na dini na Utawala pamoja na elimu.

**Kielelezo Na. 10.1**: Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa alipata alama hafifu kutokana na kushindwa kubainisha mambo mahsusi ambayo mwalimu anaweza kuyafanya katika hatua ya utangulizi anapofundisha mada ya Chimbuko la Kiswahili.

Vilevile, asilimia 33.1 walijibu swali hili na kupata alama za wastani. Baadhi yao, walibainisha baadhi ya mambo ambayo hayafanyiki kwenye hatua ya utangulizi na wengine walichambua mambo mawili kwa ufasaha badala ya manne na kupata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5.

Aidha, asilimia 9.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri kwa sababu walielewa matakwa ya swali. Waliweza kubainisha mambo matatu au manne anayoweza kuyafanya mwalimu katika hatua ya utangulizi wakati akifundisha mada ya chimbuko la Kiswahili ambayo ni *kujenga utayari kwa wanafunzi kupokea maarifa, kuuliza maswali mafupi kuhusiana na mada ya chimbuko la kiswahili, kutoa muhtasari wa somo analotaka kulifundisha (chimbuko la Kiswahili) na kuuliza maswali mafupi yanayohusiana na mada iliyopita*. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.



10. i/. Mwalimu kutambulisha somo.
ii/. Mwalimu anaweza kutumia bungua bongo baada ya kutambulisho somo kama njia ya kuvuta usikivu na utayari.
iii/. Anaweza kutumia mchoro wa chimbuko la Kiswahili kuonesho lahaja za Kiswahili
iv/. Anaweza kuuliza maswali juu ya chimbuko la Kiswahili ili kupata maarifa ya awali kabla ya kuingia hatua ya maarifa mapya.

**Kielelezo Na. 10.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kubainisha mambo anayoweza kuyafanya mwalimu katika hatua ya utangulizi wakati akifundisha mada ya chimbuko la Kiswahili.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)


Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) yaliyohitaji majibu marefu (insha) ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali mawili (2). Kila swali lilikuwa na uzito wa alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, 6 hadi 10 wastani na alihesabika kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu iwapo alipata alama 10.5 hadi 15.

### 2.2.1 Swali la 11: Uhakiki wa Kazi za Fasihi

Swali lilihusu mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Mtahiniwa alipaswa kutumia hoja tano kuthibitisha kuwa suala la uongozi mbaya ni kikwazo cha maendeleo ya jamii ambapo alielekezwa kutumia kitabu cha MALENGA WA MRIMA NIMERUDI.

Asilimia 6.3 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao asilimia 23.6 walipata alama za wastani na zaidi. Hivyo, swali hili ni miongoni

mwa maswali yaliyojibiwa vibaya. Chati Na. 11 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




***Chati Na. 11:*** *Kiwango cha kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 11.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 52 sawa na asilimia 76.5 walijibu swali hili na kupata alama hafifu ambazo ni kuanzia 1 hadi 5.5. Hii inaonesha kuwa hawakuelewa matakwa ya swali na wengine walikosa uelewa juu ya mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi* hususan katika kipengele cha *ushairi*. Baadhi yao walishindwa kuhusianisha mashairi na dhamira husika, kutaja majina ya mashairi katika kuelezea hoja na wengine walishindwa kuonesha ni jinsi gani tabia mbaya zinazofanywa na viongozi zinavyokwamisha maendeleo ya jamii na hivyo kuishia kupata alama hafifu. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika tabia mbaya zinazofanywa na viongozi kama vile *kutokuwajibika, wizi na uhujumu uchumi, tabia ya ukasuku na tabia ya ubaguzi* ilihali hazijafafanuliwa kwenye kitabu cha MALENGA WA MRIMA NIMERUDI kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Pamoja na hayo, hakuweza kuonesha ni jinsi gani tabia hizo zinakwamisha maendeleo ya jamii. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

11. Uongozi mbaya ni ile hali ya viongozi waliopewa mamlaka ya kuongoza watu wap-wanaposhindwa kuwaongoza kwa kufuata-misingi ya kidemokrasia na utu katika kuwatawala wananchi.
Katika kitabu cha MARENGA WA MRIMA kilichoandikwa na Mwinyihatibu Mohamed-amejaribu kujadili suala la uongozi mbaya kama kikwazo katika maendeleo ya jamii kwa kuangalia hoja zifuatazo.
Kuonea watu; Mwandishi Mwinyihatibu Mohamed ameonesha suala la viongozi kuwaonea wananchi kwa aina mbali-mbali kama unyanyasaji, kuwapiga pamoja na kuwanyang'anya dhuruma ambazo zina-wakandamiza na kushindwa kujikwamua kiuchumi.
Kutowajibika kwa viongozi katika kufanya kazi. Katika kitabu cha MARENGA WA MRIMA Mwandishi anajaribu kuwaonesha jinsi viongozi waliopewa mamlaka ya kuwaongoza watu na kuwatolea dibwi la umaskini-ni jinsi wasivyowajibika kwa wananchi wao. Mwandishi ametumia shairi la "nondo" kuonesha jinsi ambavyo viongozi wetu ambavyo wamekuwa wagumu katika kushughulikia matatizo yao.
Tabia ya wizi na uhujumu uchumi. Mwandishi amewaeleza viongozi wetu kama watu-ambao wapo kwa ajili ya maslahi yao katika kutafuta changamoto za wananchi na badala yao wanashiriki katika kuhujumu-

11 uchumi wa nchi yetu na kujilimbikizia
mali. Mwandishi ametumia shairi la
"wezi" kuonesha namna viongozi wetu wali-
vyo wezi ambayo ni vigumu katika ujenzi
wa maendeleo.

Tabia ya Ukasuku; Mwandishi wa
kitabu cha MALENGA WA MRIMA anaonesha
ni kwa jinsi gani viongozi wetu waliyo-
makasuku kupitia shairi la "kasuku" ambapo
mwandishi amewaonesha viongozi kama
watu wa kupiga kelele ambazo hazina
msaada kwao katika kuinua kipato-
chao ambapo hali ya ukasuku wa viongozi
wao inachangia katika kuzorota kwa maende-
leo ndani ya jamii au nchi wanazoziongoza

Tabia ya ubaguzi; Mwandishi ana-
thibitisha jinsi viongozi waliyo na ubaguzi
katika kuwaongoza watu wao ambayo-
husababisha kuzorota kwa maendeleo katika
sehemu hiyo ambayo viongozi hupeleka-
na kujenga ~~mita~~ miradi ya maendeleo-
katika sehemu zao. Hivyo mwandishi
ameyaonesha kwa kutumia ~~tabia~~ shairi
la "ubaguzi" kuonesha viongozi wanavyowa-
bagua ~~wa~~ watu wao.

Mwandishi wa ~~shairi~~ shairi la MALENGA-
WA MRIMA pia ameonesha tabia ambazo
hapendezwi nazo ambazo zinafanywa na
wanajamii kama vile tabia ya ulafi, tabia
ya choyo na tabia ya wanafunzi kufeli
mitihani kama tabia mbaya ambayo
haipaswi kuiga hata kidogo.

**Kielelezo Na. 11.1 :** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Majibu katika kielelezo Na. 11.1 yanaonesha kuwa mtahiniwa alishindwa kuthibitisha jinsi suala la uongozi mbaya linavyokwamisha maendeleo ya jamii na kupata alama hafifu.


Hata hivyo, watahiniwa 15 sawa na asilimia 22.1 walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Wengi wao, walishindwa kutafsiri lugha ya kishairi katika kuelezea hoja mbalimbali na wengine walifafanua kwa usahihi hoja mbili au tatu badala ya tano na kutokukidhi matakwa ya swali. Pia, watahiniwa wengine walishindwa kuweka sehemu ya utangulizi na hitimisho katika majibu yao.

Aidha, asilimia 1.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali hivyo kuweza kuthibitisha jinsi ambavyo suala la uongozi mbaya ni kikwazo cha maendeleo ya jamii kwa kutumia kitabu cha MALENGA WA MRIMA NIMERUDI kwa hoja 4 au 5. Hoja zilizofafanuliwa ni *rushwa*, *matumizi mabaya ya rasilimali*, *usaliti*, *udikteta na uonevu* na *matumizi mabaya ya fedha za umma* huku wakihusianisha na jamii halisi zinazowazunguka. Tofauti ya alama za watahiniwa katika kundi hili ilitokana na usahihi wa hoja na ufafanuzi uliotolewa na kila mtahiniwa. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

11. Uongozi mbaya, Ni namna ya utawala ambao ni mbaya, ambapo viongozi hutawala kwa kutumia mabavu au kujilimbikizia fedha kwa ajili ya manufaa yao. Kimsingi waandishi wa mashairi hujadili suala la ujenzi wa jamii mpya kwa kuleta mabadiliko chanya. Kwa kutumia diwani ya MALENGA WA MRIMA, kilichoandikwa na "Mwinyihatibu Muhamed" amejadili suala la uongozi mbaya kama ifuatavyo:-

Suala la rushwa, rushwa ni adui wa haki, rushwa huweza kusababisha migogoro katika jamii Kimsingi Mwandishi amejadili suala la rushwa kwa kuzingatia baadhi ya viongozi wapomadaraka Lakini wanapenda rushwa, Jinsi gani viongozi walivyoingia madarakati kwa rushwa mfano katika shairi la "rushwa" Mwandishi anajadili tatizo la rushwa ni gumu sana. Hivyo basi mwandishi anaonguyema ili kuejenga jamii mpya ni vyema kukomeshwa rushwa.

Udikteta na uonevu katika jamii, Mwandishi Mwinyihatibu, amejadili suala la udikteta kwa viongozi wake kisiri sana kwa kuwakandamiza wananchi na kufurahia keki ya Taifa mfano katika shairi la "Uongozi mbaya" mwandishi anejadili kuwa baadhi ya viongozi ni wakatili wanatumia madaraka yao kuwanyanyasa wananchi wa chini kwa sababu ya udikteta na uonevu unaofanywa na viongozi.



11. Utumiaji mbaya wa fedha za umma, mwa-
ndishi anazungumzia viongozi wanavyotumia vibaya
ya fedha mfano katika shairi la "uongozi mbaya"
kwa kuchukua rasilimali zote na kuacha wanai
nchi wakiwacha wakiishi maisha mabaya. m
wandishi anajadili kuwa ili kujenga jamii
mpya ni vyema kukomesha utumiaji mbaya
wa fedha kiujumla.
Usaliti, Mwinyihatibu amejadili kuwa
usaliti katika jamii hutokana na uongozi-
mbaya mfano amezungumzia viongozi walio
wasaliti wananchi, wakapata tabu na ku
acha wananchi wakiwa na shida. mfano, k
atika shairi la "usaliti" mwandishi anazungumzia
kuwa ni vyema kuondoa usaliti na kupinga
na ~~ubinafsi~~ rushwa ili kujenga jamii mpya
kwa ujumla.
Matumizi mabaya ya rasilimali, Kimsingi
mwandishi ameweza kujadili kuwa baadhi ya
uongozi hutumia ubaya mali za umma kama
vile madini, na vitu vingine, mfano amejadili
suala la wizi wa madini na kuuza nje
kwa sababu ya uongozi mbaya. Mwandishi
anashauri jamii ili kujenga jamii mpya ni
vyema kukemea suala la matumizi mabaya
ya rasilimali.
Hivyobasi, ni vyema kuheshimu ka
zi za fasihi kwa fasihi andishi kwa sababu
huibua mambo yaliyomo katika jamii
na kutoa ujumbe kwa jamii iliyo kusu
diwa.


**Kielelezo Na. 11.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kuthibitisha jinsi suala la uongozi mbaya linavyokwamisha maendeleo ya jamii. Aidha, alijibu swali hili kwa kufuata kanuni za uandishi wa maswali ya insha.

### 2.2.2 Swali la 12: Fasihi

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Fasihi* ambapo lilimtaka mtahiniwa abainishe sifa tano za mtambaji katika kazi ya fasihi simulizi.

Asilimia 96.4 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 90.3 ya watahiniwa waliojibu walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 12 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.





***Chati Na. 12:*** *Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 12.*

Baadhi ya watahiniwa waliopata alama za wastani ambazo ni kuanzia 6 hadi 10 ambao ni sawa na asilimia 64.8 walibainisha sifa za wastani za mtambaji kama vile *awe anazingatia muda*, *azingatie umri au jinsia* na *azingatie mpangilio wa visa*. Wengine walitaja hoja sahihi lakini wakashindwa kuzifafanua kwa kina na hivyo kupata alama pungufu.

Kwa upande mwingine, asilimia 25.5 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa wa kundi hili walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya *sifa za mtambaji* ambapo walikidhi matakwa ya swali na hivyo wakaweza kubainisha sifa za mtambaji katika kazi ya fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza sifa hizo kuwa ni *awe na uelewa mpana wa lugha na utamaduni wa jamii husika, aelewe historia na utamaduni wa jamii yake, awe anajiamini na kazi yake, awe na sifa ya ucheshi ili kunasa umakini wa hadhira, awe na*

*ubunifu wa kuichangamsha hadhira yake na pia awe na sauti inayosikika ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa*. Pamoja na hayo, mtahiniwa huyu aliweza kutoa maelezo ya kina katika kufafanua hoja na kuzingatia kanuni za uandishi wa insha. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

12. Fasihi simulizi ; ni kazi ya
sanaa ambayo inatumia Lugha kwa njia
ya masimulizi ya mdomo kufikisha uju
mbe kwa jamii iliyokusudiwa au kwa
hadhira; Fasihi simulizi ni kama vile
Hadithi, semi, ushairi na michezo ya
kuigiza.
Zifuatazo ni sifa tano za mta
mbaji wa kazi ya Fasihi simulizi
nazo ni :
Awe na sauti inayosikika; kwan
za kabisa mtambaji anapaswa awe na
sauti kuwa itakayomuwezesha kufiki
sha ujumbe uliosahihi kwa hadhira
yake hivyo sauti inatakiwa isikike
ili paweze kuwa na uelewa kwa hadh
ia yake.
Mtambaji anatakiwa ajiamini
na kazi yake; sifa nyingine ya mtambaji
anapaswa aweze kujiamini aondoe hofu
na woga ili kile alichokusudia kukifi
kisha katika hadhira yake aweze kuki
fikisha bila kuweza kupotosha mawazo
kwa hofu.
Atumie Lugha fasaha na inayoele
weka kwa hadhira; Pia mtambaji anataki
wa kuwa mjuzi wa Lugha kulingana
na utamaduni wa jamii husika. anapa
swa atumie Lugha fasaha lakini
pia iwe ni Lugha inayoelewekeka kwa
hadhira ili kwamba mawazo yaweze
kufikika.


Aelewe historia na utaratibu wa wanajamii au hadhira yake; sifa nyingine ya mtambaji yeye anapaswa aweze kutambua historia na utaratibu wa jamii namaanisha, kuanzia Lugha na utamaduni mwingine wa jamii ili aweze kuendana nayo.

Awe na uwezo wa kulitawala jukwaa; uwezo huo utajumlisha mambo yafuatayo, hisia za wasikilizaji, kuteka usikivu wa hadhira na mambo mengine ili asiwepo mtu wa kumuingilia wakati anapokuwa akiwasilisha kazi yake.

Huyo basi hizo ndizo sifa za Mtambaji wa kazi ya Fasihi Simulizi na endapo Mtambaji hatoweza kuwa na sifa zote hizo ujumbe aliokusudia kuufikisha katika jamii au kwa hadhira yake hautafikiwa...


**Kielelezo Na. 12.1 :** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na**.** 12.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kubainisha sifa tano za mtambaji wa kazi ya fasihi simulizi kutokana na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fasihi*.

Aidha, asilimia 9.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Wengi wao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya *Fasihi simulizi*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha dhima za fasihi katika jamii ambazo ni *kuelimisha jamii, kukosoa jamii, kutoa ujumbe kwa jamii, kuburudisha jamii na kusaidia kupashana habari* na mtahiniwa mwingine alishindwa kutofautisha kati ya sifa za mtambaji na sifa za mhakiki wa kazi ya fasihi kwa hoja kama vile *mhakiki anatakiwa asiwe mpondaji wa kazi za wengine, asome tahakiki za wahakiki wengine, asome kazi mbalimbali za fasihi, kuelewa historia na siasa ya jamii husika na ajue historia na mazingira yaliyomkuza mwandishi* na kupata alama 0. Vilevile, wapo baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu hoja wakaishia kuandika utangulizi tu na kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi dosari iliyosababisha kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

R Mtambaji ni mtu anayefanya kazi ya fasihimuli katika jamii kwa kutumia mdomo ili kuweza kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusiana na jambo fulani mfano inaweza ikawa kuelezea chanzo ya ugonjwa wa UKIMWI au suala la kutokithiri kwa Rushwa katika jamii. hivyo basi mtambaji ana sifa zake ~~ta~~ sifa hizo ni kama zifuatazo.

Kuelimisha jamii. hii ni mojawapo ya sifa ya mtambaji, jamii inapata Elimu kutokana na kuweza kwa mtambaji ambaye anafanya kazi ya kuelimisha jamii kutokana na kazi pale



Kukosoa jamii, hii ni miongoni
mwa sifa ambazo mtaji mtambaji
huzingatia katika kazi ya fasihi simulizi
ufano mtambaji anapoona akaangalia
fulani ovu katika jamii yake au fulani
la rushwa.
Kutoa ujumbe kwa jamii,
hii ni miongoni sifa za mtambaji
katika kazi ya fasihi simulizi, mfano
anapoona akitoa ujumbe mfano UKIMWI ni
Chanzo cha umaskini, au Ukosefu wa
Elimu ni chanzo cha ulu... wa.
akiwaeleza vyema hii yote ni muhimu
wa mtambaji
Kuburudisha jamii, hii ni
miongoni mwa sifa za mtaji mtambaji
wa kazi katika fasihi simulizi,
mtambaji hutoa maneno mazuri yenye
kufurahisha wasikilizaji kufurahia na
kuchekesha katika kama na maneno ya
mtaji mtambaji wa kazi ya fasihi
simulizi.
Husaidia kupambana na rushwa katika
jamii, mfano katika kundi la watu
wengi mtambaji anaweza akazungumza
mwa uongozi mbaya kwa njia mitambo
ambele ya uongozi wao, badala ya hapo
husaidia uongozi kubadilika.
Hivyo basi mtambaji ni mtu muhimu
sana katika jamii hii ya sasa sababu
hutumika kama mwalimu anayeweza kufundi-
sha jamii yake.


**Kielelezo Na. 12.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa alibainisha dhima tano za fasihi katika jamii badala ya sifa tano za mtambaji katika kazi ya fasihi simulizi.

### 2.2.3 Swali la 13: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili

Swali hili lilihusu mada ya *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili*. Swali lilimtaka mtahiniwa kupanga maneno kwa utaratibu wa kamusi, kisha kuonesha taarifa za kitomeo kwa kutoa maana tatu kwa kila neno (Kaa, Kata, Paa, Panda, Ua).

Swali lilijibiwa na asilimia 96.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa kuwa asilimia 86.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 13 inafafanua viwango vya kufaulu katika asilimia.





***Chati Na. 13****: Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 13.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 84.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Baadhi ya watahiniwa wa kundi hili waliweza kutoa maana tatu ya kila neno lakini hawakutoa taarifa nyingine za kitomeo kama vile aina ya neno, umoja/wingi na kuonesha kama neno hilo ni elekezi/si elekezi.Wengine waliandika kama insha badala ya kupanga maneno na taarifa zake za kitomeo kama yalivyokuwa matakwa ya swali.

Vilevile, baadhi ya watahiniwa sawa na asilimia 13.6 walipata alama hafifu kuanzia 1.5 hadi 5.5. Kati yao wapo ambao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili* hususan katika

kipengele cha *kamusi*. Wengine hawakuweza kutimiza matakwa ya swali kwa sababu walishindwa kuonesha taarifa za kitomeo katika maneno waliyopewa ambapo walitakiwa kuonesha aina ya neno, kama ni elekezi au si elekezi pamoja na kutoa maana husika.

Baadhi ya watahiniwa walitoa maana za maneno ambazo si kamilifu ingawa zilikuwa pungufu ya tatu kwa kila neno na maana nyingine zilizotolewa hazikuwa sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika maana ya *kata* kuwa ni *ngazi ya juu ya uongozi na maana nyingine ni kifaa cha kujitwishia maji* na kushindwa kuonesha neno hilo ni la aina gani, elekezi/si elekezi na kutoa maana kamili kama vile ***kata****$^{1}$ (nm) (sie) mtaa, eneo dogo kuliko tarafa na kubwa kuliko kijiji* na ***kata***$^{2}$*(nm) (sie) chombo kinachotengenezwa kutokana na zaidi ya nusu ya kifuu cha nazi na kutiwa mpini kinachotumika kuchotea maji*. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.


13. (i) paa -
- paa juu
- paa la nyumba

(ii) panda
- panda mbegu
- panda juu ya mti


(iii) kaa
- kaa la moto
- kitendo cha kukaa chini

(iv) kata
- kata kitendo cha kukata mti.
- ngazi ya juu ya uongozi
- kifaa cha kujitwishia maji

**Kielelezo Na. 13.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Majibu katika kielelezo Na. 13.1 yanaonesha kuwa mtahiniwa alishindwa kupanga maneno kwa utaratibu wa kamusi na kuonesha taarifa za kitomeo.

Vilevile, watahiniwa wachache sawa na asilimia 2.1 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15 kwa sababu walielewa kikamilifu mada ya *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili* pamoja na kuelewa vizuri matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kupanga maneno vizuri kwa utaratibu wa kamusi na kuonesha taarifa za kitomeo kwa kutoa maana tatu kwa kila neno (Kaa, Kata, Paa, Panda, Ua). Taarifa zimeonesha aina ya neno na kama neno hilo ni elekezi au si elekezi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika neno kaa kwa utaratibu wa kikamusi na kuonesha taarifa za kitomeo kama ifuatavyo: ***kaa***$^{1}$ *(nm) (-) (ma-) kipande cheusi cha kuni kilichochomwa na kuzimwa kabla ya kuwa majivu; kipande chekundu cha kuni chenye moto.* ***kaa***$^{2}$ *(nm) mnyama mdogo wa majini mwenye miguu sita au zaidi na gamba mwilini anayetembea upande upande.****kaa***$^{3}$ *(kt) (sie) weka matako au makalio juu ya kitu; keti. ~kitini, ~chini*. Aidha, mtahiniwa huyo aliandika maneno yote kwa utaratibu huo kama yaliyoulizwa kwenye swali. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.




**Kielelezo Na. 13.2 :** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kupanga maneno kwa utaratibu wa kamusi na kuonesha taarifa za kitomeo kwa usahihi.


## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalam)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) yaliyohitaji majibu marefu (insha) ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Utaalam*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali mawili (2). Kila swali lilikuwa na uzito wa alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, 6 hadi 10 wastani na 10.5 hadi 15 kiwango kizuri cha kufaulu.

### 2.3.1 Swali la 14: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilitoka katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*. Mtahiniwa alipaswa kujenga hoja tano ili kutetea kauli isemayo "Kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia ni bora kuliko kununua zana hizo".

Swali lilijibiwa na asilimia 88.9 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 99.4 ya watahiniwa walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 14 inafafanua viwango vya kufaulu katika asilimia.




***Chati Na. 14**: Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 14.*

Asilimia 79.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali na walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Zana za Kufundishia*

*na Kujifunzia*. Pia, waliweza kutetea hoja isemayo "*kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia ni bora kuliko kununua zana hizo*" kwa kueleza umuhimu wa kufaragua zana badala ya kununua kwa hoja nne hadi tano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza umuhimu wa kufaragua zana kuwa ni *kukuza vipaji katika kubuni na kutengeneza zana hizo, hupunguza gharama za manunuzi, huamsha ari ya wanafunzi kujifunza (inawamotisha wanafunzi kujifunza), hujenga mazingira ya mwanafunzi kutunza kumbukumbu* na *kujenga tabia ya ubunifu kwa wanafunzi*. Pamoja na hayo, alieleza hoja zake kwa mtiririko unaoleta mantiki pamoja na kuonesha sehemu za utangulizi na hitimisho. Mtahiniwa mwingine alieleza hoja nyingine kama vile; *hurahisisha upatikanaji wa zana za kufundishia, hurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na huchochea matumizi ya malighafi inayozunguka katika mazingira husika*. Kielelezo Na. 14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujenga hoja tano na kutetea kauli isemayo *''Kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia ni bora kuliko kununua zana hizo''*.

14. Kuyaragua Zana ni kitendo cha kutumia au
kutengeneza Zana ya kubuni itakayotumika -
katika kufundishia na kujifunzi pindi uwa-
sitishapo mawazo au maada kwa wanafunzi.
Kuyaragua tunaweza sema ni kutumia Zana isi-
yo halisi ambayo ni ya kubuni muonyowe na
siyo mawaza iwe katika mazingira yote ya
nayotuzunguka. Hivyo ni bora kuyaragua Zana ya
kufundishia na kujifunzia kutika kutumia
Zana halisi kwa sababu Zifuatazo.
Hukuza ubunifu, tunaona katika pande
zote mbili yaani mwanafunzi na mwalimu kupi-
tia Zana ya kuyaragua katika kujifunza na
kufundishia inamuongezea mwalimu uwezo
wa kubuni vitu vingine mbalimbali katika kufu-
ndisha. Pia mwanafunzi anaweza kujifunza
kubuni vitu mbalimbali kwa uelewa wake kupi-
tia Zana aliyoiona.
Husaida kutunza kumbukumbu ya kile-
kilichofundishwa, mfano endapo mwalimu atatumia
Zana halisi inayopatikana katika mazingira mfano
akitumia embe, chungwa na akatumi au faragua
Zana kwa kutumia njia yake kuonesha embe, ch-
ungwa mwanafunzi atakumbuka makini kutaka kuele
wa ubunifu wa mwalimu maana embe limezoeleka
katika mazingira ya mwanafunzi.

14. Motisha kwa wanafunzi, katika kufundisha na kujifunza mwalimu ikiwa atatumia zana ya kufaragua atakuwa motisha tosha kwa darasa lake kwa sababu inaweza kuvuta zaidi hivyo. kufanya somo lake kueleweka kwa wanafunzi.

Husaidia kujenga udadisi na uelewa wa kufikiri vizuri, kupitia zana mbalimbali ambazo mwalimu anafaragua katika kufundisha masomo darasani, wengi wa wanafunzi wanakuwa na uelewa mpana wa vitu kwa sababu zana anazotumia mwalimu inampa uwezo wa kufikiri zaidi.

Hupunguza gharama, tunaona zana za kununua huzina gharama kubwa sana wala uhitaji wa pesa kubwa ya kununua vitu. Mfano mwalimu anaweza andaa vifaa vyake kama miti, karatasi mbao ili kukamilisha zana yake kwa haraka na mtu atakaetumia zana halisi kwenda kununua dukani.

Hivyo, kufaragua zana za kufundishia ni bora zaidi kuliko kununua zana, kwa sababu ni rahisi kutumia uelewa wa kubuni vitu mbalimbali mbali na kutumia pesa kununua. Pia husaidia kumpa motisha mtumiaji kuhifadhi kumbukumbu, kuongezea uelewa na ubunifu wa mambo mbalimbali katika kujifunza.


**Kielelezo Na. 14.1**: Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kueleza umuhimu wa kufaragua zana kuliko kununua.

Halikadhalika, asilimia 20.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10 kwa kushindwa kujenga na kutetea hoja ipasavyo,

kutoa hoja zenye maelezo yasiyo kamilika, kutoa hoja 2 au 3 badala ya 5 na kushindwa kuandika utangulizi na hitimisho kikamilifu.


Watahiniwa wachache sawa na asilimia 0.6 walipata alama hafifu kuanzia 1 hadi 5.5. Baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*. Baadhi yao walishindwa kutofautisha kati ya sifa za zana, umuhimu wa kutumia zana darasani na umuhimu wa kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia kuliko kununua na kupata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika sifa za zana za kufundishia ambazo ni: *mvuto, rahisi kuhifadhi, ukubwa na kudumu* badala ya umuhimu wa kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia kama vile *hurahisisha upatikanaji wa zana za kufundishia, hurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, huchochea matumizi ya malighafi inayozunguka katika mazingira husika, kukuza vipaji katika kubuni na kutengeneza zana hizo na hupunguza gharama za manunuzi,* Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuelewa mahitaji ya swali na kupata alama hafifu.


14. "Kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia ni bora kuliko kununua zana hizo". Jenga hoja tano kutetea kauli hiyo.

Kufaragua; ni kitendo cha kumba kitu kwa kutumia vitu asilia vinavyopatikana katika mazingira fulani. Hivyo ni kweli kuwa kufaragu zana za ufundishaji na ujifunzaji ni bora kuliko hata vile za kununua zana hizo. Kauli hii inathibitishwa kwa kutumia hoja zifuatazo:

Kudumu: Zana ya kufaragua ni zana ambayo ngumu kuharibika kwa urahisi. Hivyo kupelekea kukaa kwa muda mrefu sana na kutumika kwa wakati wowote wa ufundishaji na ujifunzaji.

Ukubwa; Hizi zana za kufaragua zina sifa ya kuwa kubwa na kuonekana na hata darasa zima. Ukubwa wake ni wa asili si ule wa kupoji kwani inavyotengenezwa inatengenezwa kulingana na vile zana inavyoonekana kutoka katika kitabu au rejea.



14. Gharama: Mara nyingi zana hizi za kujaragua hazitumii kiasi kikubwa cha pesa yaani matumizi ya pesa ya kununulia zana hizi isipokuwa malighafi yanayotumika ni yale ya kuokota au kukata miti kutoka porini.

Rahisi kuhifadhiwa: Hii ni kwasababu zina kuwa ngumu kuharibika aidha kwa kuingiliwa na wadudu kama vile mchwa, hivyo kupelekea kuhifadhika kwa urahisi na kudumu muda mrefu kwa matumizi ya baadae.

Mvuto: kwa kuwa vitu vilivyo tumika kutengenezea zana ni vya asili hivyo humshawishi mwanafunzi kuzingatia sana katika kuwa makini na utumiaji wa zana hizo. Pia ule ukubwa asilia humpelekea mwanafunzi kujifunzia kwa urahisi sana.

Hivyo, ni bora kuchagua zana za ufundishaji na ujifunzaji kuliko zile za kununua kwani za kununua hazina ubora mzuri hazidumu muda mrefu, ni za gharama sana, ni rahisi sana kuharibika na kudhalilika.


**Kielelezo Na. 14.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa alieleza sifa za zana za kufundishia na kujifunzia badala ya umuhimu wa kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia kuliko kununua.

### 2.3.2 Swali la 15: Upimaji

Swali lilitoka katika mada ya *Upimaji* ambapo mtahiniwa alipaswa kueleza umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi kwa kutumia hoja tano.

Asilimia 57.6 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili lilijibiwa vizuri kuliko maswali yote katika mtihani huu kwani asilimia 99.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani na zaidi kama inavyofafanuliwa kwenye chati Na.15.




***Chati Na. 15:*** *Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 15.*

Asilimia 75.5 ya watahiniwa waliofanya swali hili walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa waliweza kueleza umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi pamoja na kuandika insha kwa kuzingatia kanuni za uandishi kama vile kuonesha sehemu ya utangulizi, kiini na hitimisho linaloshabihiana na swali husika.

Hii inadhihirisha kwamba, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi kuwa ni: *husaidia kutoa ripoti kwa wazazi, kufanya tathmini juu ya maendeleo ya wanafunzi hasa katika kubaini changamoto zinazowasababishia kufeli, kumsaidia mwalimu kuboresha mbinu au zana anazotumia katika ufundishaji, husaidia wadhibiti wa shule katika kutathmini ufundishaji pamoja* na *kuwahamasisha wanafunzi kuendelea kujifunza zaidi*. Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kuweza kueleza umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi.

15. Kwa kutumia hoja kueleza umuhimu wa-
kutunza kumbukumbu za Maendeleo ya Mwan-
afunzi.

Kumbukumbu za Maendeleo: ni nyar
aka ambazo hutunza ili kuonesha Maende-
leo ya kitu fulani, kuna umuhimu wa kutu-
nza kumbukumbu za Maendeleo ya Mwanafu-
nzi. Zifuatazo ni hoja zinazoelezea umuhimu w-
a kutunza kumbukumbu za Maendeleo ya Mwa-
nafunzi,

Kusaidia kutoa ripoti kwa wazazi: Utu
nzaji wa kumbukumbu za Maendeleo ya Mw-
anafunzi, ~~*~~ humsaidia Mwalimu kutoa Mre
jesho kwa wazazi juu ya Maendeleo ya-
watoto wao. Hii hufanyika aidha kwa nusu-
Muhula ama Muhula mzima wa Masomo.

Kumsaidia Mwalimu kufanya ta-
thmini juu ya Maendeleo ya Mwanafunzi.
Kutunza kumbukumbu za Maendeleo ya M-
wanafunzi; Mwalimu anaweza kufanya tathm
ini na kuweza kubaini changamoto zinazowa-
kabili wanafunzi na kuweza kuwasaidia katika
wakati sahihi.

Kumsaidia Mwalimu kuboresha,
Mbinu na zana anazotumia wakati wa-
wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji.
Ili Mwalimu aweze kuboresha Maendeleo ya-
Mwanafunzi ni lazima aboreshe mbinu na
zana anazozitumia darasani; hii ~~kwa~~
humsaidia katika kutunza kumbukumbu nzuri
ya Maendeleo* ya Mwanafunzi wake.

Kuwasaidia wakaguzi wa shule kufa
nya tathmini juu ya Maendeleo ya Mw
anafunzi na hivyo kubuni Mbinu/njia -
Mbalimbali (kupendekeza njia mbalimbali)
kwa ajili ya kuboresha Maendeleo ya Mwana-
funzi.

Kuwapa hamasa/Motisha wanafunzi:
Wanafunzi wanahamasika kuendelea kufany
a vizuri ili tunza kumbukumbu nzuri ya-
Maendeleo yao. hivyo wanafunzi wanaonge
za Jitihada katika Masomo.

Hivyo basi: kuna umuhimu mkub-
wa wa kutunza kumbukumbu za Maen-
deleo ya wanafunzi, kwani Mwalimu hupata
nafasi ya kutunza tabia mbalimbali za-
wanafunzi wake na kuweza kuwasaidia ku-
leta Maendeleo mazuri.

**Kielelezo Na. 15.1 :** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Majibu katika Kielelezo Na. 15.1 yanaonesha kuwa mtahiniwa alieleza umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi kwa usahihi.

Vilevile, asilimia 24.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walishindwa kufafanua vizuri baadhi ya hoja walizotoa, kueleza hoja 2 au 3 badala ya 5 na kutokuweka sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na swali hivyo kukosa alama za sehemu hizo. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama: *husaidia walimu kuchagua viongozi wa shule, kutoa zawadi mbalimbali kwa wanafunzi* na *kurahisisha ufundishaji.*

Hata hivyo, asilimia 0.3 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo walishindwa kutofautisha kati ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi, mbinu za kufundishia na kujifunzia na njia za kufanya upimaji kwa mwanafunzi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia ambazo ni: *maswali na majibu, majadiliano ya vikundi, changanya kete, Igizo dhima na matembezi ya galare* na kupata alama 0 badala ya kuelezea umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi kama vile: *husaidia kutoa ripoti kwa wazazi, kufanya tathmini juu ya maendeleo ya wanafunzi hasa katika kubaini changamoto zinazowasababishia kufeli, kumsaidia mwalimu kuboresha mbinu au zana anazotumia katika ufundishaji, husaidia wadhibiti wa shule katika kutathmini ufundishaji pamoja na kuwahamasisha wanafunzi kuendelea kujifunza zaidi*.

Vilevile, watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Upimaji* ambapo walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine hawakuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na swali hivyo kusababisha kupata alama hafifu. Kielelezo Na.15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyechanganya hoja kwa kuelezea mbinu za kufundishia na kujifunzia badala ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi.

15. Maendeleo ya Mwanafunzi, Ni maendeleo ambayo unampeleka mwanafunzi kuweza kufanya vizuri katika kazi yake za masomo na mazingira yanayo muhusu kama mbinu ya maswali na majibu, mbinu ya majadiliano, mbinu ya changanya kete, mbinu ya igizo zima, mbinu ya mafumbezi ya gatale; hizi ni mbinu ambazo mwanafunzi anaweza kupewa na mwalimu kwa ajili ya kuingalia umuhimu wa kutunza kumbu kumbu za maendeleo ya mwanafunzi ni kama:

Mbinu ya Maswali na majibu; hii inaweza kumpeleka mwanafunzi kuweza kutunza kumbukumbu za maendeleo yake katika maswali na majibu ni pale mwalimu sana katika kumuuliza mwanafunzi hivyo aweze kujibu hivyo unampatia kumbukumbu za maendeleo yake

Mbinu ya Majadiliano ya vikundi. hii ni muhimu wa kutunza kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi wanafunzi wanapojadiliana hivyo kumpa uhasin wa kuweza kuzisalimu kadhaa hivyo ataweza kupata taswira kwa kile walicho kuwa wanakijadili na kumpa kuweza kukumbuka kile alicho kisoma na kumpeleka alipendele sana somo. hivyo makundi ya majadiliano ya vikundi unampeleka mwanafunzi kuweza kupenda somo na kuwa na kumbukumbu.

Mbinu ya Changanya kete. hii ni muhimu katika kutunza kumbukumbu ya Mwanafunzi hivyo Mwanafunzi anaweza kutumia mbinu hiyo ya changanya kete kwa kuweza kutunza kumbukumbu yake na aweze kusahau kile alichofundishwa hivyo Mbinu ya changanya kete ni mbinu ambayo inaweza kutunza kumbu kumbu ya Mwanafunzi

Mbinu ya Igizo Zima. mbinu hii ambayo ni Muhimu sana katika kutunza kumbukumbu ya Mwanafunzi pale anapofanya igizo aweze kusahau kile alicho kuwa anakifanya hii inampeleka Mwanafunzi kuto weza kusahau katika kile anacho kuwa anakifanya igizo zima.


Kielelezo Na. 15.2 : Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 15.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa alishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kueleza mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia badala ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu za mwanafunzi na kupata alama hafifu.

### 2.3.3 Swali la 16: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*. Mtahiniwa alipaswa kuainisha namna bora ya kutumia ubao darasani kwa kutumia hoja sita.

Asilimia 53.2 ya watahiniwa 1,064 waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 97.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 16 inaonesha viwango vya kufaulu kwa asilimia.




***Chati Na. 16:*** *Kiwango cha Kufaulu kwa Watahiniwa katika swali la 16.*

Watahiniwa 406 sawa na asilimia 71.7 walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao, waliweza kueleza namna bora ya kutumia ubao darasani bila kutoa maelezo yanayojitosheleza. Vilevile, baadhi ya hoja hazikuwa za msingi kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza namna bora ya kutumia ubao ni: *kuandika maandishi kwa kifupi, kuchora mistari kuelekea kulia na si kwa kushuka chini* na *kufuta ubao kuanzia juu kushuka chini,* hoja zilizosababisha apate alama za wastani.

Vilevile, asilimia 25.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15 kwa kuwa walikidhi matakwa ya swali na walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*.Watahiniwa hao waliweza kuanisha namna bora ya kutumia ubao darasani pamoja na kuandika hoja zao katika mtiririko unaoleta mantiki. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja kama: *kufuta maandishi ubaoni kabla ya kutumia, kugawa ubao katika sehemu mbili au tatu kulingana na matumizi, kuandika mwandiko mzuri unaosomeka ili wanafunzi wasinakili makosa, mwalimu kutumia kioneshi wakati anapoelekeza jambo lililoandikwa ubaoni* na *mwalimu anatakiwa kusimama kwa namna ambayo haitawakinga au kuwazuia wanafunzi kuona maarifa yaliyoandikwa ubaoni* kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 16.1.


16. Ubao wa kufundishia darasani ni kifaa kinachomsaidia mwalimu pamoja na mwanafunzi kuwasilisha somo kwa ufasaha. Ubao unaweza kubainishwa kwa rangi au namna ulivyokaa. Ubao pia huwa mbele katikati ya darasa ili uweze kuonekana ipasavyo kwa darasa zima.

Zifuatazo ni mambo ya ~~ubao~~ namna bora ya kutumia ubao darasani.

Andika maandishi ubaoni kabla ya kuanza kuutumia; Hii ni namna bora ya kutumia ubao darasani katika mchakato mzima wa kufundisha na kujifunza, iki kuwa huwezi kuandika maandishi juu ya maandishi, namna ya kufuta ubao unafaa kuwe kwa ustaarabu na unadhifu kuepuka vumbi la chaki.

Kugawa ubao kulingana na umbo na matumizi; ubao unatakiwa kugawa katika pande zilizo sawa kulingana na ukubwa wa ubao huo (size) na matumizi ya ubao huo. Mfano gawa ubao katika pande tatu zilizo sawa.

Andika taarifa muhimu ubaoni kulingana na uwasilishaji wa somo. Mfano, kama ubao umegawanywa mara tatu, katikati lazima kuwe na taarifa kama mada kuu, mada ndogo, somo lenyewe na vidokezo muhimu za somo, kulia mwa ubao kuwe na taarifa za maarifa ya wanafunzi darasani na pembeni kushoto kuwe na michoro na mifano dhahiri kulingana na mada.



Mwandiko mzuri na unaosomeka na kuonekana kwa wanafunzi wote; Ili ubao uwe bora na uendane na matumizi ni lazima mwandiko wa ubaoni uwe mzuri na unaosomeka kwa wanafunzi ~~woote~~ wote darasani pia kwa kuzingatia nafasi za maandishi hayo.

Tumia kiooneshi kuonesha maandishi ubaoni; Hili ni tumizi bora la ubao darasani, kwani mwalimu au mwanafunzi anapowasilisha somo ni lazima atumie kiooneshi (pointer) kuonesha maandishi ubaoni ni si mkono wake.

Kusimama pembeni kidogo wakati wa kuandika ubaoni; Hii ni muhimu kwani inawasaidia wanafunzi kufuatilia mtiririko wa somo bila shida, hivyo wakati wa kuwasilisha somo mwalimu hatakiwi kusimama katikati ya maandishi pindi anapoandika. Hayo ndiyo matumizi mazuri ya ubao darasani.

Kulingana na namna bora mbalimbali za kutumia ubao, ubao utakuwa na mambo makubwa kwani utarahisisha somo kueleweka kwa urahisi na kupunguza kumbukumbu za kufundisha kwa wanafunzi. Hivyo sisi kama walimu tunatakiwa kuwa na maarifa ya kutosha juu ya matumizi ya ubao ili adhima ya malengo mahususi kwa kila mada ifikiwe kwa urahisi.

**Kielelezo Na. 16.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Majibu katika kielelezo Na. 16.1 yanaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kuainisha namna bora ya kutumia ubao darasani na kupata alama za juu.

Hata hivyo, asilimia 2.8 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 1 hadi 5.5 kwani hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza matumizi ya ubao badala ya namna ya kutumia ubao darasani. Hoja alizozielezea ni pamoja na: *ubao hutumika*

*kuandika tarehe, mada kuu, mada ndogo, dondoo za somo, nukuu za somo na hutumika kufanya upimaji* badala ya *kufuta maandishi ubaoni kabla ya kutumia, kugawa ubao katika sehemu mbili au tatu kulingana na matumizi, kuandika mwandiko mzuri unaosomeka ili wanafunzi wasinakili makosa, mwalimu kutumia kioneshi wakati anapoelekeza jambo lililoandikwa ubaoni na mwalimu anatakiwa kusimama kwa namna ambayo haitawakinga au kuwazuia wanafunzi kuona maarifa yaliyoandikwa ubaoni*. Katika mfano mwingine, mtahiniwa mmoja alirudia hoja moja zaidi ya mara nne katika maelezo yake na mwingine aliandika faida za kutumia ubao katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji na kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kuwa alirudia hoja moja zaidi ya mara nne.

16 Ubao ni Kifaa Kinachoandaliwa mbele
ya darasa ili kuwezesha mchakato wa ujifun
zaji na ufundishaji darasani. Zifuatazo ni
Namna bora za kutumia ubao darasani.
Hutumika kuandika Tarehe. Kabla
ya vitu vyote kuendelea mwalimu ~~huandika ta~~
huandika tarehe ya siku hiyo ubaoni upa
nde wa kulia wa ubao. Tarehe husaidia
kujua siku mada iliyofundishwa darasani
hiyo tarehe ni muhimu kwa mwalimu k
uandika kabla ya kuanza somo.
Ubao hutumika Kuandika ~~tarehe~~.
Mada kuu. Pia hutumika kuandika mada
kuu ya somo husika pia Mwalimu huandi
ka mada kuu ubaoni mada kuu ambayo
inafundishwa darasani kwa wakati hu
o. huandikwa katikati ya ubao.
Kuandika mada Ndogo. Maada ndogo
pia huandikwa ubaoni. Mwalimu huandi
ka mada ndogo ubaoni ya somo husika lina
lofundishwa kwa wakati huo ili kumweza
sha mwanafunzi kuweza kutofautisha ma
da kuu na mada ndogo. Mada ndogo hua
ndikwa chini ya Mada kuu kwa herufi ndogo
mda mwingine huandikwa peke yake kwa herufi
ndogo kama ni mada ndogo ya pili, ya tatu na kue
ndelea.
Hutumika kuandika dondoo za somo.
Mwalimu pia hutumia ubao kuandika dondoo
za somo au Hutumia ubao kuandika Ma
jibu ya wanafunzi yanayotakana na masw
ali yaliyoulizwa, Pia dondoo nyingine

16 Ni ramani, picha na michoro huwekwa na kuc
horwa ubaoni wakati wa mchakato wa ufundi
shaji na ujifunzaji darasani huandikwa kushoto.
Hutumika kuandika nukuu za somo
Ubao hutumika kuandika nukuu za somo
linalofundishwa kwa wakati huo. Mwali
mu huandika nukuu za somo ubaoni ili
wanafunzi waweze kuziandika kwenye mada
ftari yao.
Hutumika katika upimaji. Mwali
mu hutumia ubao kupima wanafunzi kile ali
chokifundisha darasani huwapima kwa kuan
dika maswali ubaoni, kuwapa mazoezi na ma
jaribio ambayo yote huandikwa ubaoni

**Kielelezo Na. 16.2 :** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa alieleza matumizi ya ubao badala ya namna bora ya kutumia ubao darasani hivyo kupata alama hafifu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa **721 Kiswahili** ulikuwa na maswali (16) yaliyotoka katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia, Ufahamu, Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili, Matamshi na Lafudhi, Maendeleo ya Kiswahili, Fasihi, Mbinu za Kufundishia na kujifunzia, Sarufi, Upimaji, Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili, Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* na *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.*

Uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo unaonesha kuwa, watahiniwa wamefanya vizuri katika mada 7 ambazo ni sawa na asilimia 58.3 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni *Zana za Kufundishia na Kujifunzia (93.8%), Ufahamu (92.8), Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili (86.4%), Matamshi na Lafudhi (85.6%), Maendeleo ya Kiswahili (85.1%), Fasihi (74.5%)* na *Mbinu za Kufundishia na kujifunzia (72.2%)*. Watahiniwa walipata kiwango kizuri cha kufaulu katika mada zilizotajwa kwa sababu walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa mada hizo na utambuzi sahihi wa matakwa ya kila swali. Halikadhalika, wengi waliweza kujieleza vizuri kwa lugha inayoeleweka, kujenga hoja vizuri katika mtiririko unaoleta mantiki pamoja na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hasa katika maswali ya insha.

Vilevile, watahiniwa walipata kiwango cha kufaulu cha wastani katika mada 4 ambazo ni sawa na asilimia 33.3 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni *Sarufi (66.9%), Upimaji (58.5%), Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili (57.1%)* na *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili (42.5%)*. Sababu za watahiniwa kupata ufaulu wa wastani katika mada hizo ni pamoja na uelewa wa wastani wa mada zilizotahiniwa, kutokuandika idadi ya hoja kulingana na matakwa ya swali na kutokufuata kanuni za uandishi hususan katika maswali ya insha.

Pia, uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa wengine walipata kiwango hafifu katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi (23.5%)*. Watahiniwa hao walipata kiwango hafifu cha kufaulu katika mada hiyo kutokana na uelewa mdogo wa mada, kutokuelewa matakwa ya swali pamoja na kutokujibu swali kikamilifu. Mchanganuo wa kufaulu kwa watahiniwa kwa mada kumefafanuliwa katika viambatisho A na B.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kwa mada ni asilimia 91.7. Hali hii inaonesha kuwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya watahiniwa walikuwa na uelewa mzuri wa mada mbalimbali zilizotahiniwa.

## 4.0 HITIMISHO

Mtihani wa Stashahada ya Ualimu ngazi ya Sekondari katika somo la Kiswahili ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Aidha, kiwango cha kufaulu kwa ujumla kilikuwa ni kizuri ambapo watahiniwa walifaulu kwa wastani wa asilimia 99.8.

Hata hivyo, katika uchambuzi huu imebainika kuwepo kwa changamoto mbalimbali zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kushindwa kufanya vizuri. Changamoto hizo ni uelewa mdogo wa matakwa ya swali, uelewa mdogo wa mada zilizotahiniwa kama vile mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, uelewa mdogo wa jinsi ya kujibu maswali pamoja na kutokuwa na ujuzi wa kujieleza kwa ufasaha hususan katika kujenga hoja zenye mtiririko unaoleta mantiki. Changamoto nyingine zilizobainika ni baadhi ya watahiniwa kushindwa kutoa mifano sahihi ya kushadidia majibu waliyotoa.

Mwisho, Baraza linatarajia kuwa, taarifa hii ya uchambuzi kuhusu majibu ya watahiniwa itatia chachu kwa walimu tarajali na wakufunzi katika kuinua kiwango cha kufaulu cha somo hili. Hii itatokana na kuelewa kasoro zinazofanywa na baadhi ya watahiniwa ambazo husababisha washindwe kujibu vizuri maswali. Aidha, taarifa hii itawasaidia walimu tarajali na wakufunzi katika kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali kwa kuona makosa yaliyosababisha kiwango hafifu cha kufaulu na kufanya marekebisho ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuzidi kuinua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika somo la Kiswahili, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Wizara inayohusika ione haja ya kuandaa warsha kwa wakufunzi ili waongeze ujuzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi* hususan katika uhakiki wa Ushairi.

(b) Wakufunzi watilie mkazo zaidi katika kuwafundisha na kuwasisitiza wanafunzi juu ya matumizi sahihi ya alama za uakifishaji sambamba na uandishi wa insha zenye mtitririko wenye kuleta mantiki. Hii itazidi kuchochea kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa ambao wamepata alama pungufu kwa kuandika insha zisizo na mtiririko mzuri.

(c) Wakufunzi na walimu tarajali waone kuwa, kuna haja ya kufundisha na kujifunza mada zote kwa kina kulingana na muhtasari unavyoelekeza.

(d) Wakufunzi wanasisitizwa kutumia mbinu na zana anuwai katika kufundisha mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi na Maandalizi ya kufundishia Somo la Kiswahili ili kuwafanya walimu tarajali kuwa mahiri zaidi katika mada hizo.

**KIAMBATISHO A**

**UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA**

| Na | Mada | Namba ya swali | Viwango vya Kufaulu (%) 40 na Zaidi | Viwango vya Kufaulu (%) Wastani | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili | 6 | 84.5 | 93.8 | Vizuri |
| | | 14 | 99.4 | | |
| | | 16 | 97.6 | | |
| 2. | Ufahamu | 7 | 92.8 | 92.8 | Vizuri |
| 3. | Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili | 13 | 86.4 | 86.4 | Vizuri |
| 4. | Matamshi na lafudhi | 5 | 85.6 | 85.6 | Vizuri |
| 5. | Maendeleo ya Kiswahili | 9 | 85.1 | 85.1 | Vizuri |
| 6. | Fasihi | 3 | 58.5 | 74.5 | Vizuri |
| | | 12 | 90.4 | | |
| 7. | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia | 2 | 72.2 | 72.2 | Vizuri |
| 8. | Sarufi | 1 | 66.9 | 66.9 | Wastani |
| 9. | Upimaji | 8 | 17.2 | 58.5 | Wastani |
| | | 15 | 99.7 | | |
| 10. | Vifaa vya Mtalaa wa Somo la Kiswahili | 4 | 57.1 | 57.1 | Wastani |
| 11. | Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili | 10 | 42.5 | 42.5 | Wastani |
| 12. | Uhakiki wa Kazi za Fasihi | 11 | 23.5 | 23.5 | Hafifu |

**KIAMBATISHO B**

## MUHTASARI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

## 721 KISWAHILI

